OFISI YA RAIS-TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI
SHULE YA SEKONDARI MGALO S.L.P 430 MAFINGA.

TAREHE **10.12.2020.**

KUMB.NA.HW/MUF/MGSS/F1……
JINA LA MWANAFUNZI----------

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI MGALO WILAYA YA MUFINDI MKOA WA IRINGA MWAKA 2021.

1.0 UTANGULIZI.

- Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha **KWANZA** katika shule hii mwaka **2021.**
- Ni matumaini yangu kuwa utaikubali nafasi hii uliyopewa na kushirikiana na wanafunzi wenzako,walimu na wafanyakazi wote katika kutekeleza malengo ya elimu.
- Kumbuka kuwa **NIDHAMU** ndiyo msingi wa mafanikio ya elimu.
- Shule hii ipo umbali wa kilomita 40 kutoka mji wa Mafinga na ipo katika kijiji cha Utosi, kata ya Sadani,tarafa ya Sadani,wilaya ya Mufindi,mkoa wa Iringa.
- Shule hii ni ya mchanganyiko (wavulana na wasichana).

2.0 KUFUNGUA SHULE.

Muhula wa masomo unaanza tarehe **11.01.2021.** Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11.01.2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **18.01.2021**, ukiwa na mahitaji ya shule kama ilivyoagizwa.

3.0 MASOMO YANAYOFUNDISHWA.

Masomo yanayofundishwa katika shule ya Sekondari Mgalo ni: Hisabati,Jiografia,Kiswahili,Uraia,Historia,Kiingereza,Fizikia,Biolojia,Kemia,Kifaranza na somo la Dini ambalo kila mwanafunzi atahudhuria vipindi vyake vya dini.

4.0 VIFAA VYA TAALUMA.

Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na vifaa vifuatavyo;

- Daftari 10 na kuendelea(counter books)
- Mkebe wa Hisabati(mathematical set)
- Kalamu za wino (pen) bluu au nyeusi
- Kalamu za Mkaa(pencel)
- Rula
- Mfuko wa kubebea daftari(begi)
- Dictionary 01 (kamusi ya kiingereza kwa kiswahili).
- Faili kubwa (box file) kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu za mitihani.

5.0 SARE ZA SHULE.

5.1 SARE YA WAVULANA

- Mashati mawili meupe tetroni ya mikono mifupi 1 na mikono mirefu 1
- Suruali mbili pana rangi ya chungwa moja na dark blue moja
- Sweta la kijani kibichi
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kisigino kifupi jozi mbili
- Tai ya rangi ya chungwa moja na dark blue moja
- Soksi rangi nyeusi jozi mbili
- Raba jozi moja kwaajili ya michezo
- Bukta ya michezo rangi Nyeusi
- Mkanda mweusi upana usiozidi nchi 2 na nusu
- Track suit rangi nyeusi kwaajili ya michezo

5.2 WASICHANA

- Blauzi mbili nyeupe tetroni ya mikono mifupi 1 na mikono mirefu 1
- Sketi mbili ndefu chini ya magoti rangi ya chungwa moja na dark blue moja
- Sweta la kijani kibichi
- Soksi nyeupe jozi mbili
- Tai ya rangi ya chungwa moja na dark blue moja
- Gauni maalumu na bukta maalumu rangi ya kwaajili ya michezo
- Raba jozi moja kwaajili ya michezo
- Viatu vyeusi vya kufunga kwa kamba vya ngozi vyenye kisigino kifupi jozi mbili
- Track suit rangi Nyeusi kwaajili ya michezo

6.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995.Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu,Sayansi,Teknolojia na Ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais-TAMISEMI yenye jukumula usimamizi na uendeshaji wa elimu.Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo katika kipindi chote cha uanafunzi wako:

- Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule.
- Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- Kutunza mali za umma.

7.0 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

- Wizi
- Uasherati na ushoga
- ubakaji
- Ulevi wa pombe,uvutaji bangi na madawa ya kulevya
- Kupiga au kupigana
- Makosa ya jinai
- Kudharau/kuharibu bendera ya taifa
- Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
- Kutoa mimba
- Kukataa adhabu kwa makusudi
- Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- Kuwa na simu ya mkononi
- Kuoa au kuolewa
- Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.

8.0. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI MWANAFUNZI ANAPORIPOTI.

- Medical examination form ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa hospitali ya serikali.
- Fomu ya mkataba/tamko la mwanafunzi kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- Fomu ya tamko la mzazi/mlezi kukiri kukubaliana na sheria,kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
- Cheti cha kuzaliwa.

KARIBU SANA MGALO SEKONDARI.

……
MWL.OSCAR P. MDEMU
MKUU WA SHULE

FOMU YA TAARIFA YA MWANAFUNZI

Jina lilioandikishwa……..
Majina mengine yanayotumiwa……
Tarehe ya kuzaliwa……..
Mahali alipozaliwa: Kijiji……Kata……
Tarafa……Wilaya…….
Jina la Baba……Yu hai/amefariki……
Jina la Mama……..Yu hai/amefariki……
Mama ana watoto wangapi……..wakike……wakiume…….
Wewe ni mtoto wa ngapi kwa mama…….
Makazi yako kwa sasa: kijiji……Kata…….
Tarafa ……Wilaya ……
Anwani ……
Jina la atakayegharamia mahitaji shuleni ……
Uhusiano wake kwako…….
Kazi yake……
Anwani yake……
Shule uliyotoka ……
Kidato ulichopokelewa kujiunga……..
Kukiwa na tatizo taarifa ipelekwe kwa……
Anwani yake……
Uhusiano wenu……..
Sahihi ya mwanafunzi……tarehe……

MKATABA WA MWANAFUNZI

Mimi……nakubali kupokea nafasi niliyopewa katika shule hii ya kibao Sekondari.
Naahidi kuwa nitahudhuria shule na vipindi vyote ndani na nje kama inavyohitajika,nitatii sharia na kanuni za shule kwa nidhamu na uaminifu wa hali ya juu,nitashirikiana na wanafunzi wenzangu , walimu, wazazi na jamii kuinua taaluma na kudumisha elimu bora.
Vitendo vyote viovu ndani na nje ya shule kwangu ni mwiko.
Jina……sahihi……tarehe……

TAMKO LA MZAZI

Mimi……..ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi…… Nakiri kusoma na kuyaelewa maagizo, sheria na kanuni za shule na kukubali mwanangu ajiunge na shule ya sekondari Kibao. Naahidi kuwa nitatumia uwezo wangu wote kumpa/kumgharamia mahitaji yote yanayotakiwa kwa muda mwafaka ili kumjengea mazingira mazuri kwa kupata Elimu bora.
Natambua kuwa kutogharamia mahitaji na kutotoa ushirikiano katika kufuatilia mwenendo na maendeleo ya mwanangu ni kukiuka wajibu wangu. Sipo tayari kuwa sababu ya usumbufu na maendeleo duni ya mwanangu.

Jina……..Sahihi……..tarehe……

MEDICAL EXAMINATION FORM

MGALO SECONDARY SCHOOL,
P. O. BOX 430,
MAFINGA.

DATE…….....

THE MEDICAL OFFICER,

……..

RE: MEDICAL EXAMINATION IN RESPECT
OF…….

I would be very grateful if you would kindly examine the above named student as his/her fitness for admission to school as a day secondary school Education under the item listed below:

……..
Head of school

Examine and certify the following items

1. EARS……..
2. EYES……..
3. BLOOD COUNT……
4. S. T. D……
5. SPLEEN……
6. CHEST……..
7. TYPHOID……
8. STOOL……
9. URINE……..
10. T. B……
11. PREGNANCE……
12. Any physical/mental defects or impairment identified……..
13. Any additional comments……

I have examined the above named student and certify his/her fit/unfit for admission to pursue secondary studies.

……..... …….

MEDICAL OFFICER'S SIGN & STAMP DATE